KUOKOLEWA KWA NEEMA YA MUNGU

Kimeandikwa na
Gary na Lynda Miller
Kimetafsiriwa na
Daudi na Iris Mwale Ogoli

Mungu anaita kitabu chake, "neno la kweli", katika II Timotheo 2:15. Mungu pia anajielezea Mwenyewe katika Tito 1: 2 kama "... Mungu, ambaye hawezi kusema uongo". Tunaweza kuamini kitabu chake kwa sababu Mungu, ambaye hawezi kusema uongo, alikiandika na ni neno la kweli.

Kijitabu hiki kitatazama mambo ambayo Mungu anasema kuhusu:

- **ufupi wa maisha**
- **uhakikisho wa kifo**
- **umuhimu wa neema ya Mungu**

Mungu anasema kwamba maisha yako ni mafupi kwa kimo. Maisha ni fupi na inapita upesi sana.

Ayubu 7:6 - 7, “Siku zangu hupita upesi kuliko chombo cha kufumia…”

Verse 7, “Kumbuka ya kwamba maisha yangu ni upepo:”

Chombo cha kufumia si kitu cha majadiliano mengi siku hizi. Tendo linalotazamwa hapa ni kama mwendo wa sindano ya cherehani wa kuenda juu na chini. Ni ghafla. Kwa kweli, inajitokeza kwa kasi kwamba jicho haliwezi hata kuona. Hivi ndivyo jinsi Ayubu anaeleza hali na urefu wa maisha yake. Maisha ya mwanadamu ni haraka kuliko chombo cha kufumia.

Merikebu ziendazo mbio ama Tai

Ayubu 9:25, 26 "…siku zangu…" Vs. 26, "Zimepita kama merikebu ziendazo mbio; mfano wa tai ayashukiaye mawindo."

Merikebu ziendazo mbio hupita haraka. Je, umeona tai akishukia mawindo? Inatendeka haraka sana hata mawindo hushikwa ghafla inakuwa chakula kwa ajili ya tai. Ni ubatili gani Bwana anatoa kwa ufupi wa maisha!

Upepo upitao

Zaburi 78:39 "Kwa maana yeye (Mungu) alikumbuka kwamba wao ni kiwiliwili; upepo upitao, wala haurudi tena.”

Hapa Mungu anaelezea maisha yako kama upepo. Upepo upitao pasipo kurudi tena. Si upepo wa kudumu kwa muda mrefu lakini upepo wa muda mfupi, upepo ulio kasi. Huu upepo ni wa muda tuu, husonga haraka pasipo kurudi.

Muda wangu ni Mfupi

Zaburi 89:47 " Kumbuka jinsi maisha yangu yanavyopita haraka.

Mungu hupima maisha yako kwa muda na anasema ni mafupi. Tunajua kwamba mtoto anafikiria ya kwamba maisha ni marefu. Mtoto huona siku zijazo na hutaka afike haraka kwa umri wa kutamani. Na wazee wanajua kwamba mtoto huyu anafanya makosa na kwamba Mungu ni wa haki. Mungu anasema kwamba muda ni mfupi. Unaweza kusema au kusikia mtu mwingine akisema, "muda huo wote umekwenda wapi?" "Umepita kwa kasi." "Siwezi kuamini unafika mwisho." Kupita haraka kwa muda inathibitisha maandiko Matakatifu kuwa ni haki.

Licha ya urefu wa maisha ya mtu yeyote, hatimaye mwishowe, atakubaliana na Mungu, jinsi muda wangu ni mfupi.

Kama Majani Hunyauka

Isaya 40:6-8 Sauti husema, “Piga kelele.” Nami nikasema, “Nipige kelele gani?” “Wanadamu wote ni kama majani, nao utukufu wao wote ni kama maua ya kondeni. Majani hunyauka na maua huanguka, kwa sababu pumzi ya BWANA huyapuliza. Hakika wanadamu ni majani.

Mungu anatueleza kwamba wanadamu wote ni kama majani. Majani hukaa kwa muda mfupi tuu. Majani hunyauka na maua huanguka. Ni maelezo ya kufedhehesha mtu. Tungependelea kama Mungu angetuambia kwamba sisi ni kama kitu cha nguvu na cha kudumu kwa muda mrefu, kama mti unaoishi maelfu ya miaka. Kumbuka, Mungu anatueleza ukweli. Tunapoona nyasi ikinyauka, tunapaswa kukumbushwa aya hizi zinazofundisha ufupi wa maisha yetu.



Kama kivuli kilichotandaa

Zaburi 102:11 Siku zangu ni kama kivuli cha jioni.

Kama kivuli cha asubuhi ni refu, tunaona kivuli cha jioni kikitandaa. Kipindi cha asubuhi kufika jioni ni nfupi. Kama jinsi kivuli hupungua, vivyo ndivyo maisha ya mtu. Mungu anaweza kutufundisha kupitia somo la kivuli.

Mvuke au ukungu unaotoweka

Yakobo 4:14 "… Maisha yenu ni nini? Ninyi ni ukungu ambao huonekana kwa kitambo kidogo kisha hutoweka.

Maisha yetu ni kama "mvuke" au “ukungu”. Fikiria kuhusu mvuke ukitoka kwa birika iliyo kwenye jiko. Mvuke huu unaweza kutufundisha kitu kuhusu urefu wa maisha yetu. Ni mfupi! Mungu anaonyesha hapa kwamba jinsi kama mvuke huonekanao kwa kitambo tu na kutoweka tena, hivyo ndivyo maisha yetu yalivyo.

Mifano yote ya urefu wa maisha yetu hufundisha ukweli huohuo. Maisha ni mafupi. Chombo cha kufumia, upepo, meli nyepesi, tai inapowinda, muda mfupi, kivuli cha jioni, nyasi inayonyauka na mvuke, ni vitu vyote vinaonyesha ufupi wa maisha.

Mungu anatueleza kwamba maisha yetu itakuwa fupi na kupita haraka sana. Wakati muda huu mfupi utaisha, itatimishwa na kifo. Mungu anaeleza sababu ya kifo. Anasema katika 1 Wakorintho 15:22, “Kwa kuwa katika Adamu watu wote hufa”

Mungu anaeleza katika Waromi 5:12, “Kwa hiyo kama vile ambavyo dhambi iliingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja, na dhambi ikaleta kifo, na kwa njia hiyo kifo kikawajia watu wote kwa kuwa wote walitenda dhambi”

Dhambi ilingia duniani kupitia Adamu. Adamu na Hawa hawakumtii Mungu. Dhambi ni kutomtii Mungu. Mungu alilaani mtu apate mauti, adhabu ya dhambi. Watu wote wako na asili ya dhambi na kifo kimepitishwa kwa watu wote.

Mwanzo 2:16-17, Mungu aliambia Adamu na Hawa, “BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu akamwambia, ‘‘Uko huru kula matunda ya mti wowote katika bustani, lakini kamwe usile matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, kwa maana siku utakapokula matunda yake, hakika utakufa.’’

Tuna soma kwamba Shetani alibadilisha neno la Mungu kwa Hawa kwa kunausha Mungu ne maneno ya Mwanzo 3:4 “4Lakini nyoka akamwambia mwanamke, “Hakika hamtakufa”.

Mungu, ambaye hawezi kusema uongo, alitimiza neno lake kwa Adamu na Hawa. Walifariki. Mungu alikuwa na vifo viwili katika mtazamo huu. Wa kiroho na wa kimwili. Dhambi yao ilivunja ushirika wao hapo na Mungu. Walikufa kiroho. Sasa walikuwa wafu kwa Mungu. Wao hawakuwa tena katika uhusiano sahihi na Mungu Muumba. Wao pia walihukumiwa kuteswa na kifo cha kimwili wakati mwingine siku zijazo. Wote wawili walikufa kifo cha kimwili.

Warumi 5:12 inasema, “kifo kikawajia watu wote .” I Wakorintho 15:22, “Kwa kuwa katika Adamu watu wote hufa, vivyo hivyo katika Kristo wote wata fanywa kuwa hai.” Watu wote katika Adamu hufa. Adamu alipitisha dhambi yake kwa binadamu wote.

Mtume Paulo anatukumbusha msimamo wetu mbele za Mungu katika Warumi. 3:23, "kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu". Pamoja na kuwa na asili ya dhambi, sisi hutenda dhambi.

Warumi 6:23, “Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu”. Mshahara wa dhambi ni mauti. Mungu anafundisha kwamba kuna vifo viwili. Kifo cha kwanza ni cha kimwili, wakati nafsi na roho zetu huondoka mwilini. Maandiko huzungumzia kifo cha pili. Kifo cha pili hufanyika wakati Mungu anahukumu mtu mwenye dhambi na kuwatupa wasioamini katika Ziwa la moto.

Waebrania 9:27 “27 Na kama ambavyo mwanadamu ameandikiwa kufa mara moja tu, na baada ya hapo kukabili hukumu”.

Warumi 6:23 tuanona neno ndogo “bali”. “Bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu”. Tunajifunza kwamba Mungu ametoa zawadi kwetu. Zawadi ni uzima wa milele katika Bwana Yesu Kristo. Mwitikio wetu lazima uwe, "Je, nipateje hii zawadi? Ninawezaje kuepuka adhabu ya dhambi yangu? Ninawezaje kuepuka hukumu ya dhambi yangu na kutangazwa kuwa na hatia na kutupwa katika Ziwa la moto milele? Je, mimi nawezaje kupokea zawadi na kuwa na uzima wa milele kwa njia ya Yesu Kristo? "

Mungu hajaweka majibu ya maswali haya kwa siri. Neno la Mungu ni mahali ambapo sisi huenda kujifunza kile ambacho Mungu amesema. Mungu daima ametoa "injili" - neno la Mungu ambalo ni kutiiwa kwa imani kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Leo katika kipindi cha neema, injili ya Mungu ambayo inaweza kutuokoa inapatikana katika maandiko yafuatayo.

Waefeso 2: 8-9, “Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; na si kwa sababu ya matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu mwenyewe. Na kwa sababu hamkuifanyia kazi, mtu ye yote asije akajisifu juu ya wokovu wake.”

Warumi 3:24, “wote wanahesabiwa haki bure kwa neema yake kwa ukombozi ulioletwa na Yesu Kristo”.

I Wakorintho 15: 3-4, “... Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama ilivyoandikwa katika Maandiko. Na kwamba alizikwa na kufufuka siku ya tatu, kama ilivyoandikwa katika Maandiko”. Ni damu ya Yesu iliyomwagika msalabani ndipo sisi tukakubalika mbele ya Mungu. Waebrania 9:22b “…pasipo kumwaga damu, hakuna msamaha wa dhambi”.

Waefeso 1:7 “Kutoka kwake, tunapata ukombozi kwa ajili ya damu yake, yaani, kusamehewa dhambi zetu; kulingana na wingi wa neema yake.”

Injili ya Mungu ni wazi na rahisi. Ni injili ya neema. Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, alizikwa na kufufuka tena. Mungu ndiye aokoaye wote na kwa kuamini. Wokovu ni zawadi kwa sababu unatolewa bure kwa mtu kwa neema ya Mungu. Wokovu hauwezi kupatikana kwa kitu chochote ufanyacho. Wokovu si kwa matendo yeyote yakujivunia. Mungu anaweza kusamehe dhambi yako na kuokoa kwa sababu Mwanawe alilipa fidia ya dhambi yako wakati alikufa juu ya msalaba wa Kalvari. Mungu sasa huokoa watu wote wale ambao wanaamini ujumbe wa injili.

Warumi 3:24, “wote wanahesabiwa haki bure kwa neema yake kwa ukombozi ulioletwa na Yesu Kristo”. Neema ni neno la ajabu na njia ya ajabu kwa Mungu ili kukabiliana na viumbe vyake. Neema inaweza kuwa kama upendeleo usiostahilika - katika uso wa kushindwa. Neema ni wema wa Mungu kwa wenye dhambi wasiostahili.

Katika Warumi 8:32 tunaona mfano wa neema ya Mungu kwa watu. “Ikiwa Mungu hakumwacha Mwanae bali alimtoa kwa ajili yetu sote, hatatupatia pamoja na Mwanae, vitu vyote??”

Mungu hakuwachia Kristo. Kristo alikwenda kwa msalaba na akafa huko kwa ajili ya dhambi yako. Hii ilikuwa ni kitendo cha neema ya Mungu kwa wanadamu wote. Wanadamu hawakustahili neema hii. Hakuna jambo nzuri katika wanadamu kujihamasisha mbele ya Mungu. Warumi 5:8- 9, “Lakini Mungu anaudhihirisha upendo wake kwetu kwamba: tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo ali kufa kwa ajili yetu. Basi, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa damu yake, bila shaka atatuokoa kutoka katika ghadhabu ya Mungu

Je unmwamini Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wako? Mungu anaangalia moyo wako. Mungu anajua kama imani yako iko katika Bwana Yesu Kristo au kama imani yako iko katika kitu au mtu mwingine. Mungu anaona moyoni.

Warumi 4:3-4, “Maandiko yanasemaje? “Abrahamu alimwamini Mungu na kwa ajili ya imani yake aka hesabiwa haki. Mtu akifanya kazi, mshahara wake hauhesabiwi kuwa ni zawadi bali ni haki yake”. Maandiko yako wazi; Mungu ataokoa kwa neema ukiamini Injili ya Kristo.

1 Wakorintho 1:18, “Kwa maana ujumbe wa msalaba ni upuuzi kwa watu wanaopotea. Lakini kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu”. Roho Mtakatifu hutumia mahubiri ya msalaba wakati huu wa neema.

Hakuna wokovu rohoni katika kuamini au kufanya jambo lolote kama yafuatayo:
• kutii Amri Kumi
• kufanya vizuri uwezavyo
• kuishi maisha mema
• kufanya matendo mema
• kutii Kanuni Kuu
• kutoa fedha kwa kanisa
• uanachama kanisa au mahudhurio
• kuomba
• kubatizwa
• kuchukua meza ya Bwana
• kuathibitisha
• kufanya toba
• au kufanya kitu kingine chochote au tendo lolote la kanisa kwa ajili yako!

Wokovu ni kwa neema ya Mungu! Sehemu yako, ni kuamini.

Warumi 11:6, “Lakini ikiwa wamechaguliwa kwa neema, haiwezekani tena wakachaguliwa kwa msingi wa matendo. Kama ingekuwa hivyo, neema isingekuwa neema tena.”

Warumi 4:5, “Lakini kwa mtu ambaye hakufanya kazi ila amemtegemea Mungu anayewahesabia haki waovu, imani yake inahesabiwa kuwa haki.”

Wokovu sio matokeo ya kuamini ujumla wa kifo cha Kristo msalabani na kazi yako ikiongezwa pamoja. Hilo ni fundisha la dini, si vile neno la Mungu hufundisha. Wokovu ni zawadi. Wokovu ni zawadi ya bure. Huwezi kufanya kazi kwa ajili ya zawadi. Zawadi ya uzima wa milele ni bure kwetu kupokea lakini iligharimu Mungu kifo cha Mwana wake wa pekee. Hatuwezi kuongeza chochote kwenye malipo yake ya dhambi zetu. Kristo alilipa yote. Waefeso 1:13, “Ninyi pia mliingia ndani ya Kristo mliposikia Neno la kweli, Injili ya wokovu wenu. Mkiisha kuamini, ndani yake mlitiwa mhuri, kwa yule Roho Mtakatifu wa ahadi mliyeahidiwa.”

Unaweza kuokolewa hivi sasa kwa kuamini injili tuu, kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi yako, akazikwa na akafufuka siku ya tatu na kwamba damu yake ni malipo ya jumla kwa ajili ya dhambi yako. Ukiamini katika moyo wako, Mungu atakusamehe na kuokoa kwa neema yake. Waefeso 1:13 inasema tulipata muhuri wa Roho Mtakatifu, kufanyika wake wa milele. Muhuri huu ni hakikisho la Mungu kwamba wokovu wa milele (Waefeso. 4:30, II Wakorintho. 1:22).

Waefeso 4:30, “Na msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye ni mhuri wenu wa uthibitisho kwa siku ya ukombozi.” 2 Wakorintho 1:22, “ametutia mhuri wake juu yetu, akatupa Roho wake mioyoni mwetu kama uthibitisho.”

Mungu huokoa na kutunza pia. Hatuwezi kamwe kupoteza wokovu wetu. Tunaokolewa na kuwekwa kwa neema ya Mungu. Mungu ndiye aokoaye sisi wote kwa neema yake na unaweza kumwamini akushike kwa neema yake.

Kumbuka, maisha ni mafupi, na usichelewe. Mwamini Kristo leo na uokolewa kwa neema ya Mungu!

Kijitabu hiki kimeletwa kwako na:

Grace Harbor Church
Gary and Lynda Miller
2822 Briarwood Dr. E.
Arlington, Hts., IL 60005
Simu: +1-847-640-8422
Marekani (USA)

Tafadhali tutembelea kwa mafunzo ya Biblia ya watoto na watu wazima

www.grace-harbor-church.org

www.lesfeldisk.org